# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

## KIKAO CHA SITA

**06 FEBRUARI, 2024**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

## KIKAO CHA SITA – TAREHE 06 FEBRUARI, 2024

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**87. MHESHIMIWA MOSHI SELEMAN KAKOSO (MPANDA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia ujenzi wa Vituo vya Afya vya Kata ya Ipwaga na Ilangu vilivyoanza kujengwa na Wananchi.

**88. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Wanawake wangapi wameshindwa kumudu *Delivery Kit* na kupewa vifaa hivyo na Hospitali au Kituo cha Afya husika.

**89. MHESHIMIWA DEUS CLEMENT SANGU (KWELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Ilemba – Kwela.

**90. MHESHIMIWA DOROTHY GEORGE KILAVE (TEMEKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Masoko chakavu ya Sterio na Tandika - Temeke.

**91. MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI CHAUREMBO (MBAGALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Mbagala na Mkuranga zitaunganishwa kwa kujenga Madaraja ya Videte, Mbagakwalu, Churwi, Tabowa na Majimatitu.

**OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

**92. MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, upi mpango wa Serikali kubadili Sera ya Uwekezaji iliyopitwa na wakati ili kuwavutia Wawekezaji nchini.

**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**93. MHESHIMIWA KASALALI EMMANUEL MAGENI (SUMVE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, lini ujenzi wa Kituo cha Ufundishaji wa Michezo katika Chuo cha Michezo Mallya utaanza kwa kuwa Mkataba ulishasainiwa.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**94. MHESHIMIWA ASYA SHARIF OMAR (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti ujenzi holela katika Miji.

**WIZARA YA MAJI:**

**95. MHESHIMIWA DAIMU IDDI MPAKATE (TUNDURU KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini mradi wa maji wa Vijiji vya Mbesa, Lijombo na *Airport* utakamilika.

**WIZARA YA FEDHA:**

**96. MHESHIMIWA NUSRAT SHAABAN HANJE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, miradi gani imetekelezwa kwa Fedha za UVIKO 19.

**97. MHESHIMIWA JANEJELLY JAMES NTATE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, lini Serikali itamaliza changamoto ya uhaba wa Watumishi katika vyombo vya TRAB na TRAT.

**WIZARA YA AFYA:**

**98. MHESHIMIWA VENANT DAUD PROTAS (IGALULA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali haioni haja ya kutoa msamaha wa matibabu kwa Wagonjwa wa Sukari na Tezi Dume nchini.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**99. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa msaada kwa Wazee ili waweze kumalizia maisha yao kwa amani.

**WIZARA YA KILIMO:**

**100. MHESHIMIWA GEORGE RANWELL MWENISONGOLE (MBOZI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itamaliza uchunguzi kwa Vyama vya AMCOS – Mbozi ambavyo havikupitiwa na uchunguzi wa awali.

**101. MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI (KARATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaboresha miundombinu ya Skimu ya Umwagiliaji katika Bonde la Eyasi.

**WIZARA YA UJENZI:**

**102. MHESHIMIWA ZAINAB ATHUMANI KATIMBA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Mkoa wa Kigoma utakamilika.

**103. MHESHIMIWA ATUPELE FREDY MWAKIBETE (BUSOKELO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali haioni haja ya kutumia teknolojia mpya ya kisasa na ya gharama nafuu katika ujenzi wa barabara nchini.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**104. MHESHIMIWA SAMWELI XADAY HHAYUMA (HANANG'):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini changamoto za mawasiliano ya simu Kata za Gesambalang, Gehandu, Simbay, Sirop na Gidahababiyeg - Hanang' zitatatuliwa.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**105. MHESHIMIWA SUBIRA KHAMIS MGALU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, upi mpango wa kuzuia Tembo kuharibu mazao na kuwadhuru Wananchi wa Kiwangwa, Bwilingu na Mkangena wanaozunguka Hifadhi ya Wami Mbiki.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**106. MHESHIMIWA NICHOLAUS GEORGE NGASSA (IGUNGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali itajenga Jengo la Mahakama ya Wilaya ya Igunga.

## IV. HOJA ZA KAMATI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

**DODOMA** **N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**06 FEBRUARI, 2024** **KATIBU WA BUNGE**